# CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA VIWANDA BIASHARA, TAASISI ZA FEDHA, HUDUMA NA USHAURI

# (TUICO)

## SERA YA ELIMU

Imeandaliwa na:
Ofisi ya Katibu Mkuu,
TUICO Makao Makuu,
Ilala Shariff Shamba,
S.L.P. 5680
DAR ES SALAAM

**YALIYOMO**

1. Vyama vya Wafanyakazi

2. Historia ya TUICO

3. Changamoto zinazokabili Chama

   i. Mageuzi ya Mfumo wa Kiuchumi
   ii. Mabadiriko ya Teknolojia
   iii. Mabadiriko ya Sheria
   iv. UKIMWI
   v. Wafanyakazi katika Uchumi usio rasmi
   vi. Afya na Usalama kazini
   vii. Mbinu za Uhamasishaji

4. Umuhimu wa Sera ya Elimu

   i. Manufaaa ya Elimu
   ii. Nafasi ya Elimu katika Kuimarisha Chama
   iii. Programmu za Elimu Zinazokusudiwa

5. Dira na Madhumuni ya Sera/Malengo ya Sera

   i. Dira
   ii. Madhumuni
   iii. Malengo ya jumla
   iv. Malengo mahususi

6. Mikakati ya Utekelezaji

   i. Muundo wa Utekelezaji wa Sera

7. Utekelezaji na Tathmini

   i. Utiliaji Mkazo katika Elimu
   ii. Utiliaji Mkazo katika Kupangilia Kazi
   iii. Usimamizi wa Utekelezaji wa Sera

## 1.0. VYAMA VYA WAFANYAKAZI

Vyama vya wafanyakazi vilianzishwa na wafanyakazi wenyewe kutokana na ukandamizaji uliokuwa unafanywa na waajiri. Mazingira ya kazi yalikuwa mabaya na wakati mwingine hatarishi, kipato kilikuwa kidogo, saa za kazi zilikuwa nyingi na hawakuwa na kauli ya kuweza kulinda na kutetea maslahi yao. Kwa maana hiyo wafanyakazi waliona umuhimu wa kuungana pamoja ili waweze kudai na kutetea maslahi yao. Ni kwa namna hiyo walianzisha vyama vya wafanyakazi ambavyo waliviendesha wenyewe kwa kutumia katiba na taratibu walizojiwekea wao wenyewe. Vyama hivi vilikua na na kuimarika, hivyo kuwa tegemeo pekee la wafanyakazi katika kulinda na kutetea maslahi na haki zao.

### 1.1 HISTORIA YA TUICO

- Chama cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO) ni mojawapo ya vyama shiriki vya TUCTA. TUICO ilianza rasmi kama chama huru cha wafanyakazi mwezi May 1995 baada ya kukamilisha uchaguzi mkuu wa kwanza.
- Januari 1996 chama kilianza rasmi kutekeleza majukumu yake ya kikatiba.
- TUICO kilipata usajili wake wa kudumu kwa mujibu wa sheria mwezi Septemba 2000.
- Chama kinaendesha shughuli zake katika mikoa yote ya Tanzania Bara (22) na kinao watendaji, vitendea kazi na ofisi katika mikoa hii.
- Kitaifa TUICO imejishirikisha na TUCTA
- Kimataifa TUICO imejishirikisha na;

  - International Federation for Chemical, Energy, Mining and General Workers Union (ICEM)
  - International Metalworkers Federation (IMF)
  - International Union of Food (IUF)
  - Union Network International (UNI)
  - Streetnet International
  - International Textile, Garments, Leather Workers Federation (ITGLWF)
- Chama kinafanya uchaguzi wa kuwapata viongozi wapya wa kuongoza chama kila baada ya miaka mitano.

## 2.0 CHANGAMOTO ZINAZOKIKABILI CHAMA

TUICO kama chama cha wafanyakazi kinakabiliwa na changamoto nyingi. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na:

- Mageuzi ya mfumo wa kiuchumi. Mageuzi ya kiuchumi yaliyofanyika na yanayoendelea kufanyika hapa nchini yamekuwa na athari mbaya kwa

chama. Miongoni mwa athari hizo ni pamoja na kupungua kwa wanachama kutokana na upunguzwaji wa wafanyakazi, kutoa nafasi kwa makampuni binafsi kufanya baadhi ya majukumu ya wafanyakazi (out sourcing) mfano, Makampuni ya kufanya usafi, kusafirisha wafanyakazi, n.k

- Baadhi ya waajiri kukiuka sheria kwa kutoruhusu TUICO kuingia maeneo ya kazi kwa ajili ya kuhamasisha wafanyakazi kujiunga na chama.
- Mabadiriko ya teknolojia ya mawasiliano ambayo yamegeuza dunia kama kuwa kama kijiji kimoja. Chama kinahitaji stadi hizi mpya katika kuendesha shughuli zake.
- Tatizo la gonjwa hatari la UKIMWI. Ugonjwa huu ni hatari na unatishia uhai wa wanachama wetu. Chama kinatakiwa kuweka mkazo katika kuwaelimisha wanachama wake juu ya madhara ya ugonjwa huu hatari na njia bora za kujikinga.
- Afya na Usalama kwa wafanyakazi. Ujio na ukuaji wa sekta binafsi haujaenda sambamba na uboreshaji wa mazingira ya kufanyia kazi. Baadhi ya maeneo ya kazi hayazingatii kanuni na masharti yaliyo katika sheria ya Afya na Usalama Na. 3 ya mwaka 2003. Ipo haja ya kuhamasisha waajiri na wafanyakazi kwa ujumla kuzingatia viwango vya Afya na Usalama vilivyo wekwa na sheria hii ili kulinda Afya na Usalama wa wafanyakazi wawapo kazini.
- Kukua kwa uchumi usio rasmi. Wapo wafanyakazi wengi wanaofanya shughuli zao katika uchumi usio rasmi. Chama kinapaswa kuingia katika eneo hili kwa madhumuni ya kuwahamasisha ili waweze kujiunga na TUICO.
- Mbinu mpya za Uhamasishaji. Watendaji wa chama wanapaswa kuelimishwa kuhusu mbinu mpya za uhamasishaji ili waweze kuongeza wanachama wapya kutoka katika sekta rasmi na uchumi usio rasmi. Hii ni muhimu ili kujenga na kuimarisha chama.
- Mabadiriko ya sheria za kazi. Viongozi, watendaji, wanachama na wafanyakazi kwa ujumla wanatakiwa kupewa Elimu ya sheria mbalimbali za kazi ili kuwawezesha kutekeleza wajibu wao kikamilifu.
- Mbinu za Majadiliano. TUICO inapaswa kuhakikisha watendaji, kamati za majadiliano zinazoundwa na chama zinapata mafunzo kuhusu mbinu za majadiliano ili waweze kuendesha majadiliano yatakayozaa mikataba ya Hali Bora kwa wanachama na wafanyakazi kwa ujumla.

## 3.0 UMUHIMU WA SERA YA ELIMU

### 3.1 MANUFAA YA ELIMU

Elimu ya vyama vya wafanyakazi ni nyenzo muhimu ya kuimarisha chama na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma. Hii hufanyika kwa kupitia njia zifuatazo:

a) Kuwashirikisha, kuwahabarisha na kuwahamasisha wanachama. Kadiri wanachamawanavyoshirikishwa katika shughuli za chama ndivyo chama

kitakapokuwa na nguvu zaidi. Wanachama watapenda kuhabarishwa juu ya sera za chama. Uelimishaji huwezesha wanachama kujuhusisha na kushiriki katika shughuli za chama.

b) Kujenga taasisi ya kidmokrasia. Programu za Elimu huwezesha wanachama kujua namna ya kutumia haki yao ya kidemokrasia ya kuchagua na kuchaguliwa na kupitisha maamuzi kidmokrasia.

c) Huwezesha wanachama kujua haki zao. Kuwaelimisha viongozi na wanachama kujua haki zao za kikatiba, kisheria, kioganaizesheni n.k. kutawapa wanachama uwezo wa kusimamia haki zao na kuhakikisha haki hizi zinatekelezwa katika sehemu zao za kazi.

d) Kuwajengea uwezo wawakilishi wa chama na kuwapa mbinu na maarifa yatakayo wawezesha kuwawakilisha wanachama vyema katika vyombo vya maamuzi na ushirikishwaji. Programu za Elimu zinasaidia sana kujenga uwezo huo.

e) Kukabiliana na changamoto za utandawazi. Utandawazi na soko huria limeleta athari kwa vyama. Hivyo programu za Elimu zitawezesha wanachama kujua namna bora ya kuzikabili athari zitokanazo na mfumo wa soko huria.

f) Kuimarisha chama. Kampeni za kuhamasisha wafanyakazi kujiunga na chama zitajenga na kuimarisha chama. Masuala ya uelimishaji na uhamasishaji katika chama huenda pamoja.

Ni kwa misingi iliyoorodheshwa hapo juu, TUICO kama chama cha wafanyakazi kimeamua kuwa na sera ya Elimu na Mafunzo itakayoongoza mfumo mzima wa utoaji Elimu ndani ya chama.

### 3.2 NAFASI YA ELIMU KATIKA KUIMARISHA CHAMA

Elimu ya vyama vya wafanyakazi ni nguzo muhimu kaitka kujenga na kuimarisha chama. Ni muhimu katika kujenga uwezo wa kufikiri na kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika maisha ya kila siku ya chama. Ili kufanikisha masuala ya Elimu ni lazima kutengeneza programu mbalimbali zitakazoendana na mahitaji ya walengwa.

## 4.0 PROGRAMU ZA ELIMU ZINAZOKUSUDIWA

TUICO inakusudia kuwa na programu za Elimu zifuatazo:-

i. Elimu ya Wawakilishi: Viongozi wote wapya watakaochaguliwa kuongoza chama ngazi ya Tawi. Kuwapa mbinu na kuwajengea moyo wa kujiamini ili waweze kuwakilisha wenzao vizuri.

ii. Elimu kwa Wawakilishi wanawake: Kuwaelimisha wahamasishaji wanawake ili waweze kuhamasisha wafanyakazi wanawake kujiunga na chama. Hii itaongeza ushiriki wa wanawake katika shughuli za chama na kuongeza uwakilishi wa wanawake katika vikao vya chama.

iii. Elimu ya Wanachama: Kuwapa uelewa wa masuala ya chama, wanachama wote kwa ujumla. Hii ni pamoja na kujua haki zao za msingi na namna ya kuzilinda na kuzitetea.

iv. Elimu kwa Wahamasishaji: Kuwajengea uwezo na mbinu za uhamasishaji, waelewe majukumu ya mhamasishaji na njia bora za kuandaa na kuendesha kampeni za uhamasishaji sehemu za kazi.

## 5.0 DIRA NA MADHUMUNI YA SERA/MALENGO YA SERA

### i. Dira

Sera hii inalenga kuhakikisha kuwa viongozi, watendaji, wanachama na wafanyakazi kwa ujumla wanaelimishwa na kupewa mbinu mbalimbali za kuwawezesha kujua haki zao za msingi na hatimaye kutekeleza wajibu wao kikamilifu.

### ii. Madhumuni ya Sera

Sera hii inalenga kufikia madhumuni yafuatayo:

- Kuimarisha umoja na ushirikiano kati ya viongozi, watendaji, wanachama na wafanyakazi kwa ujumla.
- Kukisaidia chama kiweze kuimarisha na kuboresha utoaji wa elimu kwa wanachama
- Kuhakikisha kuwa chama kinashiriki kikamilifu katika utoaji wa Elimu ya mfanyakazi kwa wanachama na wadau wengine.

### iii. Malengo ya Jumla

Malengo ya jumla ya sera hii ni kujenga ushirikishwaji kati ya wanachama na viongozi ili waweze kuelewa na kujitoa kikamilifu katika utoaji wa Elimu kwa ufanisi.

### iv. Malengo Mahususi

Kimsingi sera hii inalenga katika kufanikisha mambo yafuatayo:

- Kukiwezesha chama kufahamu umuhimu wa Elimu ya mfanyakazi na hivyo kuchukua jukumu la kugundua mahitaji ya kielimu na mafunzo sehemu za kazi.
- Kukiwezesha chama kuunda/kuboresha mtaala wa kielimu na mafunzo utakaonufaisha mahitaji ya wanachama mahali pa kazi.

- Kukiwezesha chama kujijengea uwezo wa ndani katika utoaji wa elimu na mafunzo.
- Kukiwezesha chama kuunda, kuendeleza na kutengeneza nyenzo mbalimbali za kufundishia kama vile, machapisho ya mtaala wa elimu, majarida, vitabu, maktaba na njia nyingine za kisasa za mawasiliano katika mafunzo.
- Kukiwezesha chama kuimarisha na kupanua ushirikiano wake na vyama na asasi za kimataifa katika kuimarisha na kuboresha utoaji wa Elimu kwa wanachama na wafanyakazi Tanzania.
- Kukiwezesha chama kushirikiana na asasi za ndani za umma na binafsi ambazo ni wadau katika utoaji wa Elimu ya mfanyakazi.

## 6.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI

- Kwa kutambua jukumu kuu la TUCTA katika kuimarisha umoja wa vyama vya wafanyakazi, TUICO kitashirikiana na TUCTA katika kuunda, kupanga, kutekeleza, kuratibu na kutathmini programu za Elimu.
- Kushirikiana na TUCTA katika uandaaji wa mtaala wa utoaji wa Elimu.
- Kuhamasisha waajiri washiriki kikamilifu katika kuandaa na kutekeleza programu za Elimu kwa mfanyakazi ili kuongeza ufanisi kazini.
- Kushirikiana na Serikali na wadau wengine kuunda, kuandaa na kutekeleza programu za Elimu ya watu wazima miongoni mwa wafanyakazi.
- Kushiriki kikamilifu kutafuta fedha na misaada ya kitaalamu na nyenzo ili kutekeleza sera ya Elimu.

### 6.1 MUUNDO WA UTEKELEZAJI WA SERA

- Idara ya Elimu na Uhamasishaji itakuwa ndiyo kitengo kikuu cha kuratibu masuala yote yahusuyo utoaji wa Elimu kwa wanachama na wadau wote.
- Idara ya Elimu na Uhamasishaji itasimamia utekelezaji wa sera hii katika ngazi zote za chama.
- Mkuu wa Idara ya Elimu na Uhamasishaji atawajibika kwa Katibu Mkuu katika masuala yote yahusuyo utoaji wa Elimu.
- Idara ya Elimu na Uhamasishaji itamshauri Katibu Mkuu kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa sera hii.
- Kupitia na kufanya tathmini ya programu na miongozo ya utoaji wa Elimu.
- Kufanya tathmini juu ya mtaala wa Elimu, nyenzo na mbinu za kufundishia.

## 7.0 UTEKELEZAJI NA TATHMINI

i. **Utiliaji wa Mkazo katika Elimu**

Izingatiwe kwamba katika uandaaji wa mipango kazi, chama kinalazimika kuyapa kipaumbele mahitaji, matarajio, haki na matatizo ya wafanyakazi wakati wowote mahali pa kazi.

Programu za Elimu zitazingatia changamoto zitokanazo na mabadiriko mbali mbali ya kidunia.

Elimu kwa mfanyakazi lazima ilenge kwanza katika kuwawezesha wanachama kujua, kuimarisha na kutetea haki zao kwa kushiriki katika michakato mbalimbali ya utoaji wa maamuzi yote yanayohusu ajira, mishahara, uchumi, siasa,jamii na utamaduni.

Masuala yote yanayogusa mahitaji na haki za wafanyakazi yatengenezewe programu za Elimu, kwa mfano;

- Kazi na Sheria ya Kazi
- Mbinu za Utafiti
- Mbinu za Habari na Mawasiliano
- Vigezo vya Ajira vya ILO
- Masuala ya Kijamii na Kisiasa
- Mbinu za Utatuzi wa Migogoro
- Mbinu za Ujasiriamali
- UKIMWI
- Mambo ya Kijinsia na mengineyo

ii. **Utiliaji mkazo katika Kupangilia Kazi**

Mpangokazi wa sera ya Elimu utazingatia yafuatayo;

- Tathmini ya awali ambayo itaonyesha yafuatayo;

    - Matatizo yaliyopo yanayohitaji elimu ili kuyatatua, mf; ubinafsishaji, utandawazi, UKIMWI, n.k
    - Aina ya Elimu na njia ya kuiwasilisha.
    - Makundi ya wafanyakazi na mahitaji yao kwa kila aina ya Elimu
    - Nyenzo zitakazohitajika katika kutekeleza programu ya Elimu.

- Utekelezaji utazingatia malengo na mipango ya muda mfupi na muda mrefu.

**(a) Mpango wa Muda Mrefu (Long term Plan)**

Chama kitahakikisha kinafanya kazi kwa kuzingatia malengo ya muda mrefu na malengo hayo lazima yawekwe bayana sasa.

Kadhalika programu za Elimu zilenge muda mrefu kati ya miaka mitatu hadi kumi au zaidi zikizingatia malengo, upatikanaji wa nyenzo na mabadiriko yanayoweza kutokea.

**(b) Mpango wa muda mfupi (Short term Plan)**

Hii ni mipango itokanayo na malengo ya muda mrefu ambayo inatekelezwa sasa kwa siku, wiki, mwezi, miezi mitatu, nusu mwaka au mwaka mmoja.

Tathmini ya mpango wa utekelezaji inapaswa kuwa endelevu kuanzia siku ya kwanza. Tathmini hii husaidia katika kuonyesha mapema matatizo ya kiutekelezaji, makosa ya kimipango, matukio yasiyotarajiwa na umuhimu wa kubadili mpango au kufanya marekebisho.

Taarifa za tathmini zinaweza kuwekwa kwa wiki, mwezi, miezi mitatu,miezi sita au mwaka mmmoja. Tathmini ya mpango kazi ni aina mojawapo ya mbinu za usimamizi.

**iii. Usimamizi wa Utekelezaji wa Sera**

- Ni muhimu kuweka njia ya kudumu ya kusimamia utekelezaji wa sera ya Elimu.
- Utoaji wa mara kwa mara wa taarifa ya utekelezaji wa Sera, pengine iwe ni sehemu ya taarifa ya chama ya mwaka.
- Kuweka utaratibu wa kutoa taarifa za mara kwa mara katika kila hatua ya utekelezaji.
- Utoaji wa taarifa juu ya kasoro yoyote katika utekelezaji punde tu itokeapo.
- Kuweka utaratibu wa kuwepo kwa viashiria vitakavyorahisisha upimaji wa mafanikio katika utekelezaji.